

Learning by Ear 2010

Series: Shall I tell you something? African Fables for a culture of peace

Episode: 02 The Lion, The Hyena and The Vulture

Author: Ibrahima Ndiaye

LEARNING BY EAR 2010

SHALL I TELL YOU SOMETHING?

AFRICAN FABLES FOR A CULTURE OF PEACE

EPISODE 02:

THE LION, THE HYENA AND THE VULTURE“

AUTHOR: IBRAHIMA NDIAYE

**EDITORS: YANN DURAND, STEFANIE DUCKSTEIN,
NAÏMA GUIRA**

TRANSLATION: NATALIE GLANVILLE-WALLIS

PROOFREADING: TONY DUNHAM

KISUAHELI : ERIC PONDA

Sound Clips: liegen bis Mitte Juli vor

CHARACTERS:

1. NARRATOR (male, about 40 years old)
2. SIMBA THE LION (male, about 30 years old)
3. BOUKI THE HYENA (female, about 20 years old)
4. KANTIOLI THE VULTURE (male, about 20 years old)

INTRO / PRESENTER

Hujambo msikilizaji na karibu katika makala nyingine ya Noa Bongo! Jenga Maisha yako. Habari sasa zimenea kwamba, tunakusimulia ngano kuhusu utamaduni wa Mwafrica. Ni kweli, lakini sio ngano tu! Ni hadithi zinazokusudiwa kuboresha mbinu za kukuza na kudumisha amani na maridhiano.

Je, ni vipi unaweza kukabiliana na hali ngumu ya maisha? Au ni vipi unaweza kukabiliana na ukosefu wa imani, wivu, uchoyo na ubinafsi katika jamii?

Katika kila ngano au hadithi, mtu hakosi kujifunza jambo moja au mawili ambayo yanaweza kumsaidia maishani. Leo tutasikia ngano ya Fisi na Tai, na sababu ya Fisi kuwa na mgongo uliochuchumaa, naye Tai kuwa na mgongo ulio na upara, katika hadithi hii ya Fisi, Simba na Tai.

1. MUSIC (*play as background for the entire script*)

2. NARRATOR:

Zamani za kale, palitokea Simba. Siku moja tu ya joto jingi, na huku upepo wa baridi ukivuma kutoka baharini, Simba, baada ya kula chakula cha mchana na kushiba vizuri, aliamua kubarizi kidogo nje ya tundu lake. Na hapo akaanza kupiga miayo, akapiga miayo mwishowe usingizi ukamshika na kulala. Kutokana na upepo mzuri na mchakacho wa majani, Simba huyu alianza kuota.

3. SFX: *Rustle of leaves*

4. *Lion snoring*

5. NARRATOR:

Wakati akiwa katika usingizi mzito, Fisi kwa jina Bouki, akapita karibu na mahala hapo na kuona kipande cha mzoga ubavuni mwa Simba kilichosazwa na Simba huyo. Na bila kusita akakinyemelea kipande kile kwa uangalifu mkubwa asije

kumuamsha Simba. Huyo akakiburuta hadi mafichoni mbali kidogo na Simba huyo.

6. *Lion yawns + hyena jumps in fear*

7. NARRATOR:

Lakini mara ghafla Simba akaamka na kumuita.

8. LION:

"Ah, ni wewe Fisi....! Hakuna haja ya kunigopa. Najua una njaa sana. Njoo hapa karibu usiogope kula chakula changu."

9. NARRATOR:

Lakini Fisi Bouki akawa na shaka na mwaliko huo.

10. HYENA:

"Sikuamini hata kidogo Simba."

11. NARRATOR:

Fisi akasema kwa sauti ya huzuni na kulalamika, kisha akanyamaza kwa woga, huku akitetemeka, macho yakiwa yamemtoka! Kwa sababu ya njaa aliyohisi, mbavu zilimtoka, ungeweza kuzihesabu, huku tumbo lake likinguruma...groooo...groooo kwa sababu ya njaa. Lakini bado aliogopa mwaliko wa Simba tu!.

12. LION:

"Kwanini unaogopa? Mimi nimeshiba! Woga wako utakufanya ukose meng! Huyu paa ni mtamu sana, sioni kwanini nimle peke yangu na siwezi kummaliza. Bora tujumuike pamoja, kwani hakuna kitu cha furaha duniani kama kula pamoja au kugawana na mwenzako. Kwa hivyo karibu tule kisha tunaweza kuwa marafiki."

13. NARRATOR:

Kwa sababu ya ulafi wake, fisi alikubali mwito huo kwa haraka japo kwa woga.

14. LION:

“Kula.... Endelea kufurahia chakula chako”

15. NARRATOR:

...Simba akamkaribisha mgeni wake. Na baada ya kupata imani ya kuketi meza moja na Simba, Bouki akaanza hadithi kuhusu hali ngumu ya maisha inayokumba kijiji chao. Akajisahau na hata kuanza kuwaonea huruma maskini zaidi katika kijiji hicho. Lakini kinyume kabisa hungeweza kumuamini anayosema.

Wawili hao walikula pamoja kwa furaha, na ghfla

Tai Kantioli ambaye alikuwa akiwatazama kwa mbali na hamu kubwa akatokezea.

16. SFX: *Cry of a vulture*

17. VULTURE:

“Habari zenu. Naona mnafurahia chakula chenu. Naomba mnitupie mabaki ya chakula chenu baada ya maliza. Nahisi njaa na tumbo langu linanguruma tangu asubuhi kwa sababu ya njaa.”

18. LION:

“Kwanini tukupe mabaki? Karibu ule nasi Kantioli. Nakualika kwa moyo mkunjufu! Bado kuna chakula cha kututosha sisi sote watatu!”

19. NARRATOR:

Mwenyeji akawakaribisha wageni kwa usodai sana. Lakini

ukarimu wa Simba huyu kisha ukazua mjadala mkubwa ambao haujawahi kushuhudiwa kabla.

20. VULTURE:

“Ni furaha yangu kujumuika nawe hapa! Ungejua jinsi ninavyoteseka kwa upweke ungenionea huruma! Lakini lazima nikiri umaskini wangu, nachukia maisha ninayoishi. Mimi ni ndege wa kawaida tu ambaye hushinda mchana kutwa juu ya mti kuwaza umaskini wangu na kusubiri mabaki ya chakula.”

21. HYENA:

“Umezua hoja nzuri sana kudhihirisha utu wako. Endapo upweke unaweza kuua, basi ningekuwa kaburini hivi sasa.”

22. LION:

“Naam, na hiyo ni kumaanisha kwamba sote tunakabiliwa na matatizo sawa, kwani miayo ninayopiga wakati niko mpweke pia mimi ningekuwa nimekufa na kuzikwa mdomo wazi.”

23. NARRATOR:

... Akaongeza Simba, huku wote wakikubaliana kwa masikitiko makubwa.

24. LION:

“Basi kama hali ni hiyo hiyo kwa kila mmoja wetu, kwanini tusiishi pamoja katika tundu hili langu?”

25. NARRATOR:

Fisi na Tai wakaridhia wazo hilo. Lakini kwa masharti kwamba waheshimu mali ya wengine. Na hapo wote wakahamia katika tundu la Simba.

26. ALL: The animals moving in (*played by actors: pushig, saying ahh, ohh*)

27. NARRATOR:

Hata hivyo lakini, urafiki au uhusiano huo haukudumu kwa muda mrefu:

Baada ya siku chache, Simba alirudi nyumbani na Paa mkubwa zaidi kuliko yule wa mwanzoni na walikuwa na chakula kingi zaidi cha kuwatosha. Kisha kama kawaida akawaalika rafiki zake kuja kula naye. Siku hiyo kulikuwa na baridi, hivyo akaamua kuwasha moto. Lakini kabla ya kuanza kupika, akashikwa na usingizi.

28. LION: *Lion yawning, snoring*

29. NARRATOR

Simba alianza kipiga miayo, kukoroma kwa sauti na hata kuota. Lakini Fisi hangeweza kuvumilia njaa aliyokuwa nayo. Na mwishowe akaamua kutoroka na Paa kwenda kumla peke yake mafichoni. Punde alipotia meno yake kwenye mnofu wa Paa huyo, Simba akaamka.

30. LION/HYENA: *The lion strikes the hyena with his paw*

31. HYENA: *The hyena takes off screaming*

32. NARRATOR:

Simba alimpiga fisi kwenye sehemu zake za makalio kuanzia kiunoni na kuangukia makaa ya moto. Kishindo chake kilitawanya makaa hayo ya moto na kuteketeza manyoya kwenye kichwa cha rafiki yake Tai .

33. SFX: *Flutter of Vulture*

34. NARRATOR:

Kwa hofu Kantioli alitoroka tundu hilo la Simba akifuatwa nyuma na Fisi ambaye mate yalikuwa yakimdondoka. Kutokana na kishindo hicho, Fisi alipata majeraha ya moto kwenye makalio, na kuumia mgongo, ndio sababu kila umuonapo fisi akitembea ameinamia nyuma kana kwamba anatafuta mahali pa kupoesha makalio yake yaliyoteketea siku hiyo. Tai akapoteza manyoya mgongoni.

35. MUSIC

Na hadi hapo ngano yetu inafika ukingoni, kwani fumbo mfumbie mjinga mwerevu atalifumbua.

OUTRO:

Oooohhhh. Ni masaibu ya Simba, Fisi na Tai, ngano inayomalizika kwa huzuni nyingi! Je, maoni yako ni yapi kuhusu ngano hii? Ulishawahi kujikuta katika mazingira ambapo kila mmoja anang'ang'ania umiliki wa rasilimali chache zilizopo? Na iwapo yamekukuta basi, je, umeshuhudia mmoja akitaka kuwakandamiza wengine? Ama unadhani huu ndio msingi wa maisha ya amani? Tuma maoni yako kupitia email yetu lbe@dw.world.de au ukipenda kusikiliza tena kipindi hiki na vingine vya

Learning by Ear 2010

Series: Shall I tell you something? African Fables for a culture of peace

Episode: 02 The Lion, The Hyena and The Vulture

Author: Ibrahima Ndiaye

Noa Bingo tembelea mtandao wetu wa www.dw-world.de/lbe. Hadi wakati mwengine Kwaheri kwa sasa!

END